# Misingi ya Mfumo Dume katika Jamii: Mfano wa Wahusika wa Kiume katika Tamthilia ya *Mke Mwenza*

*Mutungi Boaz*
*Chuo Kikuu cha Makerere, Uganda*

**Ikisiri**

**Harakati za kumkomboa mwanamke dhidi ya utawala wa kuumeni ni jambo ambalo limedumu tangu miaka ya 1960 ambapo shughuli za Tapo la Ukombozi wa Wanawake zilianza kupamba moto kote duniani. Katika taaluma ya fasihi, nadharia mahususi ya ufeministi iliundwa kwa lengo la kutumia fasihi kama jukwaa la kumuinua na kumkomboa mwanamke. Mojawapo ya malengo ya nadharia hii ni kuwahimiza wanafasihi kuunda mhusika kielelezo wa kike, anayesifika, na mwenye uwezo katika nyanja mbalimbali za kijamii. Je, harakati za Tapo la Ukombozi wa Wanawake pamoja na utekelezaji wa nadharia ya ufeministi yameathirije mfumo dume? Je, wahusika wa kiume bado wababe? Je, mfumo dume umepungua au unakithiri? Makala haya yanalenga kujibu maswali haya kwa kuchunguza sifa na tabia za wahusika wa kiume katika tamthilia ya 'Mke Mwenza' ya Nyaigotti-Chacha (1982). Kwa kutumia mkabala wa ufeministi wa Kiafrika, utafiti wetu umegundua kwamba mila, imani na mienendo ya kijadi, na hata ya kisasa inaendelea kumdhalilisha mhusika wa kike, huku akikwezwa mhusika wa kiume. Kwa jumla, mhusika wa kiume bado anadhihirisha mamlaka katika jamii.**

**Maneno Muhimu:** Mfumo-Dume, Misingi, Uke Wenza, Ufeministi wa Kiafrika

## Utangulizi

Mfumo dume unarejelea mamlaka na uongozi wa kuumeni ambapo mienendo na nyanja zote za jamii zinaendelezwa kwa misingi na masilahi ya binadamu wa kiume kwa kumchukulia kama mtu wa hadhi ya juu, mwenye nguvu na uwezo zaidi kuliko binadamu wa kike. Mfumo dume una asili yake katika familia za kijadi ambapo baba au mzazi wa kiume kimsingi ndiye alikuwa kiongozi na mwenye mamlaka yote katika familia. Baadaye, maana hiyo ilipanuliwa hadi kushikiria mila na taratibu nyingine za jamii. Dipio (1998) anaeleza kuwa katika jamii za kidume, vyeo na ngazi muhimu kitabaka huchukuliwa na wanaume. Kwa upande mwingine,

mwanamke hubaki binadamu duni na nafasi yake huwa ya nyuma au ya pembeni, asiye na umuhimu mkubwa, isipokuwa katika kumhudumia mwanamume. Waasisi wa ufeministi wanaamini kuwa mfumo dume umechangia sana katika kumtweza mwanamke.

Akizungumzia uhusiano hasi baina ya mfumo dume na unyanyasaji wa wanawake, Inhorn (1996:4) anasema:

> Katika udume rasmi, vijana wa kike huozwa katika familia zinazoongozwa na baba za waume zao. Huko, vijana hao hujikuta sio tu chini ya wanaume wote bali hutawaliwa pia na wanawake walio wakubwa zaidi, hasa mama-wakwe zao. Na bila fursa ya kurithi chochote kutoka upande wa baba zao, mabibi-arusi hawa wabichi huingizwa katika familia za waume zao kama binadamu wanyonge, wasio na mbele wala nyuma. Basi, matumaini yao pekee katika jamii hii ya kidume huyaelekeza tu kwenye watoto (hasa watoto wa kiume) watakaowazaa.[1]

Kwa jumla, mfumo dume unachukuliwa kama kiini cha unyanyasaji na ubaguzi dhidi ya wanawake katika hali zake mbalimbali katika ndoa na familia, na katika nyanja kadhaa za kijamii, kisiasa na kiuchumi.

## Harakati za Kifeministi dhidi ya Mfumo Dume

Utabaka na ubaguzi wa kijinsia dhidi ya mwanamke uliwafanya wahisani kuunda Tapo la Kimataifa la Ukombozi wa Wanawake[2] ili kupigania usawa na haki ya wanawake duniani. Aidha, wanafasihi waliunda nadharia ya ufeministi na mojawapo ya malengo yake ni kuwasawazisha wanadamu wote licha ya utamaduni, maumbile na jinsia zao (Njogu na Chimerah, 1999). Kuna mikabala mbalimbali ya ufeministi na makala haya yametumia mkabala wa Kiafrika ambao unasisitiza upekee wa hali na mazingira ya mwanamke wa Barani Afrika pamoja na kujadili vipengele vya utamaduni wa Kiafrika bila ya hukumu wala kuviangalia kama visivyo halali (Mekgwe, 2003).

Kwa mujibu wa Chilisa (2012), mkabala wa Ufeministi wa Kiafrika umejengwa kwa mihimili mitatu. Kwanza, ni uchangamani wa kimuktadha na kiutamaduni. Mhimili huu unaeleza kwamba muktadha, tamaduni pamoja na watu

[1] Tafsiri yetu ya: *Under classic patriarchy, young girls are married into households headed by their husband's father. There, they are subordinate not only to all the men, but also to the more senior women, especially their mothers-in-law. Often having no claim on their father's patrimony, young brides enter their husbands' households as effectively dispossessed individuals who can establish their place in the patriliny only through child bearing (especially by producing male offsprings).*

[2] Tafsiri yetu ya *International Women Liberation Movement.*

wa Kiafrika ni changamani kwani mazingira yenyewe ni ya aina mbalimbali kiasi kwamba hukuna usawa wala mfanano wa jumla. Hivyo, ufafanuzi wake lazima uwe thabiti na halisi kuliko kuangaliwa kijumla. Mhimili wa pili unafafanua ushirikiano na kutegemeana baina ya wanaume, wanawake na watoto, pamoja na baina ya walio hai na waliofariki. Katika hali hii wanaume pia hushiriki katika harakati za kupinga udhalimu wa kijinsia. Mhimili wa tatu unahusu umuhimu wa ari na umoja katika kujikomboa huku pia wakijiangalia kama jumuiya moja wasiofaa kuumizana kijamii. Kwa hivyo, mkabala wa ufeministi wa Kiafrika unasaidia katika kuelewa namna wahusika wa kike na wa kiume wanavyotangamana katika muktadha thabiti wa kijinsia. Mkabala huu unalenga kuwainua wanawake huku pia ukishirikisha wanaume kama jumuiya moja ya binadamu wanaotarajiwa kutegemeana.

**Muhtasari wa Tamthilia ya *Mke Mwenza***

Tamthilia ya *Mke Mwenza* inasawiri mikinzano ya kitamaduni baina ya mila za jadi na za kigeni, kama vile ubepari na ubinafsi. Mgogoro huo wa kimila unasababisha hali ya mvutano katika jamii. Kwenye kiwango cha familia, hakuna maafikiano yoyote bali ni ugomvi, utengano, chuki na mauaji. Katika Ufunguo[3] wa tamthilia Mtabiri[4] wa dini ya kiasili anakiri kwamba licha ya kuongezeka kwa elimu na maarifa "kuna mambo ambayo yametushinda" (uk. 1).

Wanajamii wameshindwa kutambua, na baadaye kutatua shida zao. Baadhi ya changamoto za jamii anazojadili mwanatamthilia ni uchoyo, utabaka, kuwadhulumu wanyonge, na kutoheshimiana. Utendaji wa tamthilia hasa unajikita katika wahusika wakuu wawili, Chahe na Boke, ambao ni mume na mke. Kupitia wahusika hawa tunatambua hasa namna taratibu za jamii ya kale zilivyoathiriwa na mfumo mpya wa kibepari katika muktadha wa ndoa ya ukewenza. Chahe na Boke wana watoto wanne wa kike, jambo ambalo halimridhishi Chahe kwani mke wake hajamzalia mtoto wa kiume, ambaye angerithi mali yake na kuendeleza jina la ukoo. Hivyo, Chahe lazima ajaribu "karata nyingine" kwa kumuoa mke wa pili, Robi, ili apate kumzaa mrithi (uk. 7). Boke hawezi kuvumilia kuolewa pamoja na mke mwenza ambaye atagawana kwenye mali yake na Chahe. Punde si punde, Boke anamuua Chahe na kuendelea kutumia mali hiyo ovyo hadi mzuka wa

[3] Ni "dondoo tangulizi" linalosaidia kutoa muhtasari wa yaliyomo katika Onyesho fulani au tamthilia kwa jumla.

[4] Mtabiri anatumiwa kama mbinu ya kutangazia au kutolea fununu mambo ambayo yatafuata. Anabashiri yaliyo usoni ili akili ya hadhira iwe tayari kupokea lolote litakalojiri. Ni upenyezi wa mtunzi katika uendelezaji wa kazi.

marehemu Chahe, wenye nguvu za kiume unapomwangamiza mwishoni mwa tamthilia.

**Misingi ya Mfumo Dume katika *Mke Mwenza***

Msingi ni "chanzo au chimbuko la kitu fulani; ni kitu au jambo la mwanzo ambalo ni la muhimu kuliko mengine yoyote yaliyo juu yake" (BAKITA, 2015: 738). Katika makala haya, neon "msingi" linatumika kueleza desturi, imani, vitendo, mienendo na asasi za kijamii ambazo zinaendeleza mfumo dume. Katika tamthilia ya *Mke Mwenza*, wahusika wa kiume wanathibitisha uwezo maalumu na mamlaka katika jamii, mambo ambayo wanatumia kujiimarisha na kujinufaisha wenyewe. Mwanzoni mwa tamthilia, amri na ukali yanayoashiria mamlaka ya kiume yanajitokeza katika maneno ya Chahe, akimwamsha mkewe, Boke:

> **Chahe:** Boke! Boke! Njoo upesi! --- (*Anaita tena*).
> Boke --- Ebho! Unadhani wewe ni nani---?
> --- Amka! (uk. 2)

Katika jamii inayoongozwa kwa minajiri ya mfumo dume, mume ndiye 'simba' wa nyumba na kila angurumapo, lazima mke atii bila kusita. Neno na uamuzi wake ni kama sheria. Hivyo, Chahe anadhihirisha sifa za kidume anapomwita mke wake bila ya 'samahani' wala 'tafadhali.' Boke anaitikia mara tu kwani mke anatarajiwa kudhihirisha upole na unyenyekevu anapotangamana na mume wake. Ni kwa namna hii, ndipo asasi ya ndoa inajengwa na kuendelezwa kwa imani na utamaduni unaomkandamiza mwanamke. Wamitila (2002) anasisitiza kuwa ndoa imejengwa kwenye imani ya uwezo mkubwa alio nao mwanamume ambapo mwanamke anachukuliwa kama chombo. Hivyo, imani ya uwezo mkubwa anaozungumzia Wamitila ndio msingi imara wa mfumo dume katika tamthilia ya *Mke Mwenza*. Hata hivyo, mwanatamthilia anakejeli mfumo dume pale Chahe anaposhindwa kudhibiti mawazo na mahitaji yake na kuishia katika ulevi. Ulevi hakika si suluhisho la shida za binadamu. Kila anapozidiwa na mawazo, Chahe anakimbilia pombe kama "dawa" au suluhisho (uk. 3). Ijapokuwa Boke anapinga ulevi wa mume wake, bado anawajibika katika kumpatia mume wake "dawa" yake kwani mke hana budi kutii amri ya mume hata iwe mbovu vipi, na huo ndio udume maradufu. Vilevile, mwanatamthilia anawalinganua Chahe na Boke kimakusudi ambapo Chahe ni mlevi, mpotovu, asiyefaa kuigwa; huku Boke akiwa ni muungwana, mwenye akili timamu na mawazo yenye tija. Ajabu ni kwamba ushauri mwafaka anaotoa Boke ni jitihada bure kwa sababu Chahe anapuuza kila asemacho:

> ***Boke:*** --- Chahe mume wangu, mimi nakustahi sana na nina-
> thamini nyumba yetu na maisha yetu, lakini kelele zako
> hizi za asubuhi kila siku hazitusaidii chochote. Isitoshe
> watoto wakitusikia haitakuwa vizuri. (uk. 4)

Kutokana na upuuzi wa Chahe, Boke anatokea kama mhusika mwema ingawa ni mnyonge ambaye anahurumiwa na msomaji au hadhira kwa jumla. Katika hali hiyo, mtunzi anakashifu mienendo ya mfumo dume katika jamii. Ukandamizwaji na unyonge wa mwanamke unadhihirisha utawala wa kiume kama mfumo usiotilia maanani ukweli na haki. Hivyo, Chahe ni kielelezo wazi cha mfumo dume, mwenye uwezo na mamlaka tele huku binafsi akidhihirisha mawazo duni. Baadaye tunagundua ya kuwa sababu ya wasiwasi wake Chahe ni kutokuwa na mtoto wa kiume. Hivyo, lazima amuoe mke mwingine ili aweze kutimiza matarajio yake ya kumpata mtoto wa kiume. Hii ni kwa mujibu wa mila na desturi za jamii yake ambayo imejengwa na kutawaliwa kwa misingi ya mfumo dume. Mtoto wa kike pia anadhalilishwa kama mama yake. Chahe anawarejelea watoto wake kama "genge la majike." (uk.7). Maelezo ya aina hii yanasisitiza hoja kwamba mwanamke ni kiumbe duni na dhaifu kwa maoni ya jamii ya kidume. Vilevile, asasi ya ndoa inalinganishwa na mchezo wa karata. Chahe anataka kuachiliwa ili ajaribu "karata nyingine" na bila shaka Boke anaitikia kwa uchungu na hasira:

**Boke:** *(Kicheko cha uchungu)*: Unasemaje? Ati karata
nyingine! Maanake mie nimekuwa karata mbovu
sana, sio? Tangu hapo umeishadhamiria kuoa mke
mwingine kumbe--- wala huoni haya kuja nilaghai
mie wazi wazi? --- Karata mpya! (uk. 7)

Hii inadhihirisha wazi namna jamii ya kidume inavyomchukulia mwanamke kama chombo; anayeweza kutupiliwa mbali wakati wowote mume wake anapopenda, bila ya kujali haki wala mchango wake katika jamii. Uchungu mtupu wa aina hii sio kitu rahisi kuvumiliwa na binadamu yeyote kama inavyothibitishwa na Boke.

Genge, rafiki yake Chahe, anahisi kwamba "kukosa mrithi ni mkosi wa kutosha" lakini anaongezea kuwa "mambo mengi yamebadilika humu duniani" (uk. 10). Hapa tunaanza kufikiria namna mabadiliko hayo yanavyoathiri mila na mienendo ya jamii. Kuna ukinzani baina ya utamaduni wa kikale na ule wa kisasa, huku pia kukiwa na haja ya kuitikia vilivyo ili kutatua mgogoro huo. Genge anamweleza rafiki yake kuwa:

**Genge:** --- Zamani, mke na watoto walikuwa ni mali ya mbari,
na mali ya matajiri pia ilitumiwa kwa maslahi ya jamii
nzima. Mambo sivyo yalivyo sasa - wengi wetu siku hizi
wanaishi kibinafsi… Na mkeo naye kama yeyote yule,
yaonesha amekumbwa na hii enzi ya 'vuta nikuvute.' (uk. 10)

Kwa mujibu wa Genge, mambo kama ukewenza hayawezi kustawi katika jamii inayoongozwa kwa misingi ya ubinafsi bila ya kuzusha misukosuko na mitafaruku. Huo pia ndio msimamo wa Boke kwani yeye mwenyewe ameshaugua wazimu na uraibu juu ya pesa na mali kwa jumla. Kwa msingi uo huo Boke amepoteza utu

pamoja na ubinadamu wake. Yeye hana huruma hata kwa mumewe, tena babake watoto wake. Basi, anaona afadhali kumuua mumewe badala ya kupoteza au kugawana mali yao na mke mwenza.Hata hivyo, ubinafsi pamoja na hali ya "vuta nikuvute" huchochea ubaguzi na unyonyaji zaidi hasa kwa walio wanyonge na wasiojiweza, hususan wanawake na watoto. Hivyo, mfumo dume umestawi katika hali ya kibepari kwa sababu yote yanahusisha utabaka. Ubinafsi ndio unamfanya Chahe kutaka kuoa mke wa pili, yaani kuweza kutetea na kuzidisha mali hiyo hiyo. Pia, Chahe anataka kuingia Bungeni kwa sababu hizo za kibwanyenye. Aidha, Genge anaeleza namna mfumo dume unavyowanyonya na kuwadunisha wanawake kwa kuwafanya vibarua na vyombo vya kazi. Anasema:

> **Genge:** --- Mimi nimeoa wake wengi, bali sababu zilizonifanya kuoa sio kama hizo zako. Niliwaoa wale wasichana badala ya kuwaajiri. Kama ujuavyo katika mashamba yangu yote siandiki vibarua; wake zangu na watoto wao wanatosha --- (uk.11)

Ingawa Genge anajiangalia kama mwenye hisani aliyewasaidia kwa kuwaoa "wasichana" hao badala ya kuwaajiri, bila shaka huu ni unyonyaji kwa wanawake walio wanyonge. Genge anawatumia wake zake pamoja na watoto wake ili kuzidisha mali, uwezo na mamlaka yake. Hali hii huendelea kumfanya mwanamke kubaki chini na nyuma na vile vile kumtegemea mwanamume. Akieleza juu ya hali hiyo ya unyonge wa mwanamke katika mazingira ya kitabaka na ya kibepari, Mukobwa, (1984:55), anaeleza kuwa:

> Katika jamii ya kikabaila na kibepari nafasi ya mwanamke hudunishwa hadi kuangaliwa kama chombo cha uzalishaji mali. Na kwa sababu jamii huwa inaongozwa kwa misingi ya kidume, mwanamume kwa kawaida hujihisi kuwa hummiliki mke wake ---

Kwa hiyo, Genge anamwakilisha bepari wa kidume anayeendeleza maslahi yake kwa kuwatumikisha wake pamoja na watoto wake, maskini wasiojiweza. Kilingana na maelezo yake Chahe, wanaume "wengine huoa wasichana wabichi kwa sababu wake zao wakubwa huwa wamezeeka" (uk. 11). Jambo hili linadhihirisha uchoyo, upendeleo, unafiki na ubinafsi wa mfumo dume. Isitoshe, Chahe amekwishatoa uamuzi kwani Boke atake asitake, lazima amwoe mke mwingine. Vilevile, anajigamba juu ya uhuru wa kufanya uamuzi huo, eti kwa sababu "ninatumia madaraka yangu nikiwa mkuu wa nyumba hii" (uk. 9). Imani pamoja na mitazamo ya jamii za kidume ndiyo msingi unaomwongoza Chahe kujiamini namna hii. Kwa kweli mawazo haya siyo yake kibinafsi, bali ni ya jamii nzima; ni utamaduni na pia mtazamo wa jamii nzima ya Kimara. Kwa msingi huu basi, mienendo ya kibinafsi na kibepari imesaidia katika kuendeleza unyanyasaji na unyonyaji kwa wanyonge hasa wanawake na watoto na vilevile kuendeleza na

kustawisha mfumo dume. Vilevile, asasi ya ndoa, hasa uoaji wa wake wengi, huendeleza udhalilishaji pamoja na ubaguzi dhidi ya mwanamke.

Udume pia unadhihirishwa pale Chahe anapomwelezea Robi, "karata mpya," kama "msichana aliyeumbika vizuri na kisomo chake si haba…" Haya hutukumbusha kuwa mwanamume ndiye mwenye mamlaka ya kutoa vigezo vya uzuri au ubaya wa mwanamke, yaani urembo na elimu ndiyo manufaa anayelenga. Inastaajabisha kuwaona maskini wake wenza, Boke na Robi, wanapokutana mara ya kwanza wanavutana na kutukanana vikali. Ni vita vya wanyonge, wenyewe kwa wenyewe na Chahe ndiye anawatuliza kwa kebehi:

**Chahe:** Ngoja, ngoja, ngoja, ngoja. Wacheni! Nyote mu wanawake, sitaki. Wewe Boke umetunukiwa kuwa mke wangu wa kwanza. Hata hivyo, hatukuweka nadhiri yoyote kuwa utakuwa mke wangu wa pekee. (uk. 14)

Maneno haya hujitokeza kama msimamo wa mwanatamthilia, Chacha, ambaye pia ni mwanamume, tena mwanamume aliyelelewa na kukulia katika mazingira ya jamii ya kidume. Kwanza, Chahe anaeleza kwamba Boke na Robi "nyote mu manawake" na kwa hivyo basi, hawana idhini kuamua ni nani aolewa na lini. Hii ni kwa sababu katika jamii ya kidume, mwanamke hana hiari wala uhuru kuhusu mambo ya ndoa. Na kwa mujibu wa lugha baguzi ya kijinsi, mwanamume ndiye "anaoa" huku mwanamke akingoja tu "kuolewa". Basi, lugha hutumiwa kama chombo cha kuimarisha utawala wa kiume.

Chahe anazungumzia "nadhiri" ya ndoa ili kubainisha mwelekeo wa mfumo dume juu ya hali ya mwanamke katika jamii ya kidume. Anadai kwamba mwanamume ana uhuru wa kuoa idadi yoyote ya wanawake anaowataka kwa sababu "hakuna ubaya kuoa mke wa pili au wa tatu ama zaidi" (*Mke Mwenza*, uk. 15). Kinyume na mila hiyo, wanawake wanatarajiwa *kuolewa* tu na mwanamume mmoja wakati wowote ule. Hivyo, Chahe anatekeleza tu mila na desturi za jamii yake ya kidume. Vilevile, maneno ya Chahe yanamulika kiwango ambacho wanawake wa Kimara wamefikia katika harakati zao za kujikomboa kutoka udhalilishaji wa mfumo dume. Ni muhimu wanawake watambue adui yao wa msingi na mivutano kati ya Boke na Robi unaonyesha kuwa ukombozi wa mwanamke bado haujaimarika. Udume bado unakithiri na ndiyo maana Boke na Robi wanapigana wenyewe badala ya kushirikiana dhidi ya adui yao, Chahe. Mfumo dume pia unadhihirika katika mahusiano baina ya Boke na kipenzi chake, Sigawa. Anapompigia simu mara ya kwanza, Boke anamwambia:

**Boke:** --- Hata huna haja ya kuuliza; mali ni yako --- *(Anacheka kwa furaha).* Ahsante... Nakusubiri kwa hamu njoo upesi bwana naugua --- (uk. 16)

Maneno haya ya kinafiki humsawiri Boke kama mwanamke mchafu na kahaba anayefanya vitendo vya ngono nje ya ndoa. Kutokana na maneno ya aina hii, jamii haina budi kuendelea kumdhalilisha mwanamke ambaye kwa kiasi kikubwa hajiheshimu. Na kwa sababu ya vitendo vyake vya namna hii, nia zake zinashukiwa na msomaji. Kwa kumsawiri hivi, mtunzi anatekeleza matakwa ya mfumo dume hasa imani ya kwamba mwanamke ni kiumbe asiyeweza kusawazishwa na mwanamume.

Sigawa, kupitia maelezo ya jukwaani anatambulika kama "kijana mwenye umri wa miaka ishirini na tano", huku Boke akiwa mwanamke wa makamo na ambaye kwa kawaida anamzidi umri na akili, na vile vile anatarajiwa kumwelekeza na kumshauri vilivyo. Hata hivyo, tunaona Sigawa anayatawala maisha na fikira zake Boke. Kumtegemea mwamume ndivyo wanavyolelewa wanawake na pia ndiyo imani ya jamii wanamokulia. Boke anapojihusisha na Sigawa katika vitendo vya ngono, anajipuuza huku pia akithibitisha kutowajibika. Sifa za aina hii huwafanya wanawake kutoheshimiwa na kutoaminiwa katika jamii. Boke anatamani sana kumshawishi Sigawa na kwa sababu hiyo, yuko tayari kumgawia mali ya mume wake, Chahe, ili ashawishike kwa urahisi. Isitoshe, Boke amekwisha sahau hata watoto wake na marehemu Chahe ambao alikuwa ameapa kwamba hatawaacha kunyanyaswa na mke mwingine. Ajabu ni kwamba sasa ameanza kuwanyanyasa watoto hao mwenyewe. Aidha, Sigawa ameanza kumtawala Boke kiasi ilhali mtazamaji anajua kuwa Sigawa ni kijana asiye na mbele wala nyuma. Hakuna budi kuwa sifa ya kipekee anayotumia Sigawa katika kumpumbaza Boke ni jinsia yake ya kiume.

Katika kumsawiri na kumhukumu namna hii mhusika Boke, mwandishi anadhihirisha msimamo wake mwenyewe huku pia akiwasilisha mawazo na imani za jamii inayotawaliwa kwa misingi ya mfumo dume. Yaani, yeye mwenyewe amekulia na kulelewa katika jamii baguzi ya kidume ambayo haimtilii maanani mwanamke. Labda hii ndiyo sababu baadaye Boke mwenyewe anakiri kwamba nyumba au familia haiwezi kuwepo ama kutambulika bila ya mwanamume. Akirejelea jambo la urithi, Boke anamweleza Sigawa kuwa:

> **Boke:** Unajua mila na sheria za Wamara hazimruhusu msichana kurithi mali ya baba yake. Ikiwa mke huyo wa pili atazaa mtoto wa kiume basi nyumba yangu itakuwa ni kama haipo tena. (uk. 18)

Kwa hivyo, misingi imara ya udume katika jamii ni imani zilizojengwa kwa mila, desturi na tamaduni za wanajamii wenyewe. Tena shida zaidi ni kuwa hata mwanamke hana budi kuamini na kutekeleza imani zizo hizo kama tunavyomwona hapa Boke. Maana yake ubaguzi wa kijinsia unaojitokeza katika mfumo wa kidume unageuka kuwa ukawaida wa mambo yote katika jamii.

Ulipaji wa mahari ni kiini kingine kinachoendeleza mfumo dume katika jamii. Hoja hii inaungwa mkono na maneno ya Mtabiri, akizungumzia hali ya Robi baada ya kifo cha 'mumewe', Chahe:

**Mtabiri:** Robi binti wa Kerata
Mambo yatakulemea
Kwa sheria ya Wa-mara
Wewe ni mke wa Chahe
Au nasema uwongo? … (uk. 24)

Hili ni thibitisho la dhuluma kwa wanawake, kutokana na imani pamoja na vitendo vya kidume. Mke anadhulumiwa na kunyanyaswa kwa sababu mahari inapolipwa huwa amedunishwa hadi kugeuka chombo kilichonunuliwa sokoni ili kumfaidi na kumnufaisha mume na familia yake kwa ujumla. Zaidi ya hayo, tunaelezwa kwamba mahari hiyo ililipwa kwa "baba" na sio kwa "wazazi" wake Robi. Hivi ndivyo hali ilivyo katika familia ya kidume; yaani watoto huwa ni wa mwanamume (baba yao) na sio wa mwanamke (mama yao) ingawa yeye ndiye anamzaa, anamlea na anamkuza mtoto. Kwa majukumu na kazi zote hizi za kuwalea watoto, kamwe si haki kwamba mke huwa anamtumikia tu mume wake. Hii ndiyo sababu mkabala wa ufeministi wa Kiafrika unasisitiza dhima ya mwanamke kama mama katika jamii. Vilevile Mogosi, akiongea na mume wake, Sagini, husisitiza kwamba, Robi ameshakuwa mmojawapo wa familia yao kwani mahari imelipwa tayari. Mogosi pia anaeleza athari ya ulipaji mahari kwa familia ya mwanamke hata ikiwa mchumba amefariki kabla ya kuozwa kwenyewe:

**Mogosi:** [Marehemu] Chahe alikuwa amelipa ng'ombe
kwao [Robi] na kidesturi ataishi na sisi *(Kituo)*.
Isipokuwa nina wasiwasi --- watoto wa siku hizi! (uk. 26-27)

Robi mwenyewe, akiongea na mama-mkwe wake, Mogosi, anakiri kunaswa na desturi hii ya ulipaji wa mahari na namna desturi hiyo inavyowanyanyasa wanawake:

**Robi:** --- Mbona una wasiwasi mama? Popote nitakapo-
kuwa si bado nitakuwa mke wa Chahe tu? (uk. 31)

Shida yenyewe ni kwamba desturi hii inalemea upande mmoja; kwani mwanamume huwa na uhuru wa kumwoa mke mwingine wakati wowote ule, ilhali maskini mwanamke haruhusiwi kumwendea mume mwingine hata baada ya kufiwa na mume wake. Hii ni desturi iliyo hasi na baguzi kabisa dhidi ya mwanamke ambayo haifai kuendelezwa hasa kwa kumnyima haki binadamu wa kike.

Mwishowe, tunaona pia kwamba hata baada ya kifo, mwanamume bado huendelea kushikilia nguvu na uwezo wake wa kidume. Mkabala wa ufeministi wa Kiafrika unaeleza kwamba kuna ushirikiano baina ya binadamu walio hai na wale waliofariki. Hivyo, kutokana na nguvu maalumu za kidume, mzuka wa Chahe

unalipiza kisasi kwa kumwadhibu Boke kutokana na mauaji na uhalifu aliotenda, kama anavyoonyesha mwanatamthilia katika maelezo ya jukwaa:

> --- *Ghafula mzuka wa Chahe unarudi na kuchukua mzuka wa Boke. Mizuka hii miwili inacheza, mara mzuka wa Chahe unaanza kuupiga mzuka wa Boke.* (uk. 39)

Hii inadhihirisha namna udume ulivyoimarika hata katika hisia, matendo na maisha ya wanajamii kwa jumla. Mfumo dume umekuwepo katika jamii za jana, upo sasa, na inaelekea utaendelea kuwepo.

**Hitimisho**

Tamthilia ya *Mke Mwenza* ni kielelezo mwafaka cha mfumo dume. Tamthilia yenyewe inasawiri na kuelezea misingi ya mfumo huo ambayo inajikita katika imani na desturi za kijamii ambazo zinawabagua na kuwadhalilisha wanawake. Desturi hizi zinaendelezwa wazi katika mambo ya urithi hasa kwa kutomthamini mtoto wa kike. Katika kutekeleza imani na desturi hizo, wahusika wa kiume hasa Chahe na baba yake, Sagini, wanajitokeza kama wababe katika utawala wa aila zao ingawa vizazi vyao ni tofauti. Kizazi cha kina Chahe kinatawaliwa na ubinafsi na uchoyo ambayo pia yanambagua mwanamke katika mahusiano ya kijinsia.

**Marejeleo**

BAKITA (2015). *Kamusi Kuu ya Kiswahili* (Toleo la 2). Dar es Salaam: Longhorn

Chacha, N.C. (1982). *Mke Mwenza*. Nairobi: Heinemann.

Chilisa, B. (2012). *Indigenous Research Methododlogies*. Washington DC: SAGE Publications.

Dipio, D. (1998). *Theory and Criticism of Literature*. Department of Distance Education, Makerere University – Kampala.

Mekgwe, P. (2003). *Theorizing African Feminism: The "Colonial" Question*. Paper presented at the University of Botswana, Dept of English Seminar Series.

Mukobwa, M. (Mh) (1984). *MWAMKO* (Toleo la 2). Jarida la Kiswahili, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Njogu, K. na Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Revikin, J. na Ryan, M. (Wah) (1998). *Literary Theory: An Anthology*. Oxford: Blackwell.

Wamitila, K.W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.